



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**



TAARIFA KWA UMMA

**MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSHS. 507,000,000 ZA UJENZI WA
MIUNDOMBINU ELIMU YA AWALI NA MSINGI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, **Bi Umy Wayayu** anutaarifu Umma kuwa amepokea fedha kiasi cha **Tshs. 507,000,000 (Shilingi Milioni 507)** kutoka Serikali Kuu kupitia program ya BOOST mwaka 2023/2024

Fedha hizo zilizopokelewa ni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya elimu ya awali na msingi katika kata za Shibula na Bugogwa,

Kati ya fedha hizo **Tshs. 351,500,000.00 (Shilingi Milioni 351.5)** ni kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya yenye mkondo mmoja katika kata ya shibula.

Fedha kiasi cha Tshs, 155,500,000.00 zitatumika kujenga **madarasa mawili ya awali ya mfano, matundu 12 ya vyoo na vyumba vitatu vya madarasa** katika shule ya msingi Kayenze ndogo iliyopo kata ya Bugogwa.

Mkurugenzi Umy Wayayu kwa niaba ya uongozi wa Ilemela anatoa shukrani za dhati kwa **Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya kujifunzia na kufundishia Ilemela.

Violencea S. Mbakile
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela
26 Juni, 2024

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, S.L.P 735, Mwanza.

Simu Na. +255(28) 2981196, Nukushi:+255(28) 2981196, BaruaPepe:md@ilemelamc.go.tz,
Tovuti: www.ilemelamc.go.tz